



## Jinsi Emma Anavyomfuata Yesu

Emma anamfuata Yesu Kristo kwa kuwa mkarimu. Anataka kuwa rafiki wa wote! Anapenda kuzungumza na watu na kucheza michezo na watoto wengine. "Mimi ninapenda kucheza na marafiki zangu na kuwapa zawadi kwa sababu nawapenda watu," Emma anasema. Wakati mwingine anatengeneza kadi kwa ajili ya marafiki na familia.

Emma pia humsaidia mama yake kuwatunza kaka zake wachanga ambao ni mapacha. Yeye husaidia kupika vyakula kwa ajili ya familia yao na kuwalisha kaka zake wachanga kwa chupa zao. "Ninahisi vizuri na furaha ninaposaidia. Ninajua kwamba Baba wa Mbinguni atanibariki," Emma anasema. ●



### Wewe Pia Unaweza Kumfuata Yesu!

Ni kipi umefanya ili kumfuata Yesu? Andika na utueleze! Nenda kwenye jalada la nyuma ili uone namna ya kufanya hivyo.



Halo!



### Kuhusu Emma

**UMRI:** miaka 10

**KUTOKA:** Shefa, Vanuatu

**LUGHA:** Kingereza, Kibislama, Kifiji

**MALENGO:** 1) Kwenda misheni. 2) Kuwa rubani

**MICHEZO:** Kuogelea na karaoke

**FAMILIA:** Emma, Mama, Baba, dada mmoja na kaka wawili.

### Mambo Ayapendayo Emma

**HADITHI YA KITABU CHA MORMONI:** Lehi na familia yake wakiondoka Yerusalemu (ona 1 Nefi 2)

**DESTURI YA LIKIZO:** Kugawa peremende na kadi kwa marafiki kwa ajili ya Pasaka

**MATUNDA NA MBOGAMBOGA:** Ndizi, matufaa, machungwa, tikiti maji, letusi, karoti

**RANGI:** Waridi

**WIMBO WA DARASA LA WATOTO:** "Families Can Be Together Forever," (Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 188).

# Kumfuata Yesu huko Vanuatu